

GRADE 1 END TERM 3 MARCH 2022
KISWAHILI

JINA

Nambari ya mwanafunzi Jinsia: Mvulana Msichana

Jina la shule Msimbo wa shule

Mwalimu ajaze jedwali hili baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi

Sehemu ya	Alama	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
1 Kusikiliza na kuzungumza					
2 Kusoma					
3 Sarufi					
4 Kuandika					

SEHEMU YA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

1. Mwalimu hutumia nini kuandika ubaoni?
2. Madawati hutumikaje darasani?
3. Wanafunzi wanapoenda nyumbani na vitabu, wao huviweka wapi?
4. Mwanafunzi anaweza kutumia kifutio chake vipi?
5. Chati huwekwa wapi darasani?

SEHEMU YA 2: KUSOMA

Zoezi la 1: Kusoma kwa sauti.

Shule yetu inaitwa shule ya msingi ya Mavuno. Iko katika kaunti ya Peponi karibu na mto Riva. Tuna walimu saba na wanafunzi ishirini katika darasa letu. Ninaipenda sana shule yetu.

Alama 10

Zoezi la 2: Kusoma kwa ufahamu

Soma hadithi na ujibu maswali yafuatayo.

Ngina ni msichana wa Gredi ya kwanza. Anasoma katika shule ya Kilimani. Anaishi na nyanya yake katika kijiji cha Moroto. Ngina hafanyi vyema masomoni lakini huchoza piano kanisani kila Jumapili.

11. Msichana aliyetajwa anaitwa _____.
12. Msichana mwenyewe yuko katika Gredi ya _____.
13. Shule ya msichana huyo inaitwa _____.
14. Kanisani, msichana huyo huchoza _____.
15. Kijiji kilichotajwa kinaitwa _____.

SEHEMU YA 3: SARUFI

Andika sentensi hizi katika umoja au wingi.

16. Kalamu yangu inaandika. _____.
17. Wazazi wetu wamekuja. _____.
18. Meza yangu imevunjika. _____.
19. Nguo zetu ni mpya. _____.

Pigia mistari viambishi vya nafsi.

20. Mimi ninasoma gazeti.
21. Sisi tunaogelea bwawani.
22. Mimi ninapenda mayai.

Andika wingi wa sentensi hizi

23. Ninataka kuandika. _____.
24. Ninapika chai. _____.
25. Ninaenda shuleni. _____.

SEHEMU YA 4: KUANDIKA

Andika sentensi hizi upya.

26. Nilienda kumtembelea rafiki yangu.
_____.
27. Alikuwa akicheza mpira uwanjani.
_____.
28. Alifurahi aliponiona kwao.
_____.
29. Tulicheza uwanjani pamoja.
_____.
30. Ilikuwa ni siku ya furaha.
_____.